-

# USHUHUDA WA KIKRISTO KATIKA ULIMWENGU WA DINI NYINGI

## MAPENDEKEZO YA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Pontifical Council for Interreligious Dialogue

World Council of Churches

World Evangelical Alliance

## UTANGULIZI

Utume ni sehemu ya uhai halisi wa Kanisa. Kutangaza neno la Mungu na kulishuhudia kwa ulimwengu ni wajibu wa lazima kwa kila mkristo. Wakati huo huo ni lazima kufanya hivyo kwa kufuata misingi ya injili, kwa heshima kubwa na upendo kwa wanadamu wengine.

Kwa kutambua hali za migogoro iliyopo kati ya watu na jumuiya zinazoamini dini tofauti na tofauti zilizopo za tafsiri ya ushuhuda wa kikristo, Baraza la Kipapa la Mazungumzano na dini zingine (Pontifical Council for Interreligious Dialogue - PCID), Baraza la Makanisa Ulimwenguni (World Council of Churches - WCC) na, kwa mwaliko wa WCC, Shirikisho la Ulimwengu la Makanisa ya Kiinjili (World Evangelical Alliance - WEA), walikutana kwa kipindi cha miaka mitano kutafakari na kutoa hati hii itakayosaidia kama mapendekezo ya utaratibu wa ushuhuda wa wakristo kote duniani. Hati hii hailengi kuwa tamko la kiteolojia juu ya utume bali kuelezea masuala halisi yanayohusiana na ushuhuda wa kikristo katika ulimwengu wa dini nyingi.

Lengo la hati hii ni kuyahimiza makanisa, mabaraza ya makanisa na mawakala wa utume kutafakari juu ya namna za utendaji sasa na kutumia mapendekezo ya hati hii kwa ajili ya kuandaa, pale inapofaa, miongozo yao kwa ajili ya ushuhuda na utume miongoni mwa watu wa dini mbalimbali na miongoni mwa wale wasiokiri imani yoyote. Ni matumaini yetu kuwa wakristo kote duniani wataisoma hati hii kwa mwanga wa mazoea yao katika kuishuhudia imani yao kwa Kristo, kwa maneno na matendo.

## MSINGI WA USHUHUDA WA KIKRISTO

1. Kwa wakristo ni heshima na furaha ya kueleza matumaini waliyonayo na kufanya hivyo kwa upole na heshima (rej. 1Petro 3:15).

2. Yesu Kristo ni ushuhuda wa juu kabisa (rej. Yohane 18:37). Mara zote ushuhuda wa kikristo ni kushiriki katika ushuhuda wake, ambao unajidhihirisha kwa njia ya kuutangaza ufalme, utumishi kwa jirani na zawadi ya kujitoa binafsi kikamilifu hata kama tendo hilo la kujitoa linapelekea kwenye msalaba. Kama Baba alivyomtuma Mwana kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ndivyo waamini wanavyotumwa katika utume kushuhudia kwa maneno na matendo upendo wa utatu wa Mungu mmoja.

3. Mfano wa mafundisho ya Yesu Kristo na ya Kanisa la mwanzo yanapaswa kuwa dira ya utume wa kikristo. Kwa milenia mbili, wakristo wamekuwa wakitafuta njia ya Kristo kwa kushiriki habari njema ya ufalme wa Mungu (rej. Luka 4:16-20).

4. Ushuhuda wa kikristo katika ulimwengu wa dini nyingi unajumuisha kutumia mazungumzano na watu wa dini na tamaduni tofauti (rej. Matendo 17:22-28).

5. Katika muktadha mwingine, ni vigumu kuishi na kutangaza injili, ama kwa kukwamishwa au kwa kuzuiwa, lakini bado wakristo wanaagizwa na Kristo kudumu kiaminifu katika mshikamano wao kwa wao katika kumshuhudia (rej. Matayo 28:19-20; Marko 16:14-18; Luka 22:44-48; Yohane 20:21; Matendo 1:8).

6. Kama wakristo wanatumia mbinu zisizofaa katika kutekeleza utume kwa udanganyifu na kwa njia za kulazimisha, watakuwa wanaisaliti injili na wanaweza kusababisha mateso kwa wengine. Kupotoka huku kunadai toba na kunatukumbusha hitaji letu la kuomba neema endelevu ya Mungu (rej. Warumi 3:23).

7. Wakristo wanathibitisha kuwa pamoja na kwamba ni wajibu wao kumshuhudia Kristo, mwisho wa yote uongofu ni kazi ya Roho Mtakatifu (rej. Yohane 16:7-9; Matendo 10:44-47). Wakristo wanagundua pia kwamba Roho anavuma anakotaka kwa namna ambazo hakuna mwanadamu anayeweza kuzidhibiti (rej. Yohane 3:8).

## KANUNI

Wakristo wanaalikwa kuzingatia kanuni zifuatazo kila wanapotafuta kutimiza utume wa Kristo kwa namna inayofaa, hususani katika muktadha wa mahusiano ya kidini.

1. **Kutenda katika upendo wa Mungu**. Wakristo wanaamini kuwa Mungu ni asili ya upendo wote na, kwa hiyo, katika ushuhuda wao wanaalikwa kuishi maisha ya upendo na kuwapenda jirani zao kama wanavyojipenda wenyewe (rej. Matayo 22:34-40; Yohane 14:15).

2. **Kumfuasa Kristo**. Katika nyanja zote za maisha, na zaidi sana katika ushuhuda wao, wakristo wanaalikwa kufuata mfano wa mafundisho ya Yesu Kristo, wakishiriki upendo wake, wakimtukuza na kumheshimu Mungu Baba katika nguvu ya Roho Mtakatifu (Yohane 20:21-23).

3. **Fadhila za kikristo**. Wakristo wanaitwa kuishi kiadilifu, kwa upendo, huruma, unyenyekevu na kushinda kiburi, kujishusha na kuwa na kiasi (rej. Wagalatia 5:22).

4. **Matendo ya utumishi na haki**. Wakristo wanaalikwa kutenda kwa haki na kupenda kwa wema (rej. Mika 6:8). Wakristo wanaalikwa zaidi kuwahudumia wengine na kwa kufanya hivyo kumtambua Kristo katika kaka na dada walio wadogo (rej. Matayo 25:45). Matendo ya utumishi, kama vile kutoa elimu, huduma ya afya, misaada na matendo ya haki na utetezi ni sehemu ya msingi katika kuishuhudia Injili. Kujinufaisha kupitia hali za umaskini na uhitaji wa wengine hakuna nafasi katika utume wa kikristo. Wakristo wanapaswa kupinga na kujizuia na namna zote za kushawishi, iwe ni kushawishi kwa fedha au zawadi, wanapofanya matendo ya utumishi.

5. **Utambuzi katika utume wa uponyaji**. Kama sehemu ya msingi ya ushuhuda wa injili, wakristo wanatoa huduma ya uponyaji. Wakristo wanaalikwa kutambua kwamba wanapotoa huduma hizi wanapaswa kuheshimu kikamilifu hadhi ya mwanadamu na kuhakikisha kuwa udhaifu wa watu na uhitaji wao wa kuponywa havitumiwi.

6. **Kupinga vurugu**. Wakristo wanaalikwa kupinga aina zote za vurugu katika ushuhuda wao, iwe ni za kisaikolojia au za kijamii, ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya mamlaka. Wakristo wanapinga vurugu, ubaguzi na ukandamizaji unaofanywa na dini yoyote au mamlaka ya kisekulari, ikiwa ni pamoja na kunajisiwa au kuharibiwa maeneo ya ibada, sanamu na vitabu vitakatifu.

7. **Uhuru wa dini na kuabudu**. Uhuru wa kuabudu, ikiwa ni pamoja na haki ya kukiri imani na kuiishi wazi wazi, kuisambaza au kubadili dini, ni matokeo ya hadhi hasa ya mwanadamu ambayo ina msingi wake katika mwanadamu kuumbwa kwa sura na mfano wa Mungu (rej. Mwanzo 1:26). Kwa hiyo, wanadamu wote wana haki na wajibu sawa. Pale dini yoyote inapotumika kwa minajili ya siasa au pale madhulumu ya kidini yanapotokea, wakristo wanaalikwa kutoa ushuhuda wa kinabii kwa kupinga matendo kama hayo.

8. **Kuheshimiana na mshikamano**. Wakristo wanaitwa kujitoa kushirikiana na watu wote kwa kuheshimiana, kukuza kwa pamoja haki, amani na manufaa ya wote. Ushirikiano baina ya dini mbalimbali ni jambo la muhimu katika wajibu huu.

9. **Heshima kwa watu wote**. Wakristo wanapaswa kutambua kwamba Injili inatoa changamoto inayotajirisha tamaduni. Hata pale injili inapotoa changamoto kwa baadhi ya nyanja za tamaduni, wakristo wanaalikwa kuwaheshimu watu wote.

Wakristo wanaalikwa pia kutambua mambo ambayo kwayo injili inayapa changamoto.

10. **Kupinga ushuhuda wa uongo**. Wakristo wanapaswa kuongea kwa heshima na unyofu; wanapaswa kusikiliza ili kujifunza na kuelewa imani na namna za imani za watu wengine, na wanahimizwa kutambua na kuenzi kile kilicho cha kweli na kizuri katika imani hizo. Wajibu wowote au ukosoaji unapaswa kufanywa katika hali ya heshima, na kuhakikisha hawashuhudii uongo juu ya dini nyingine.

11. **Kusaidia mang'amuzi binafsi**. Wakristo wanapaswa kutambua kwamba mtu kubadili dini yake ni hatua ya uamuzi ambayo inapaswa kusindikizwa na muda wa kutosha wa tafakari na maandalizi, kupitia hatua inayohakikisha uhuru binafsi.

12. **Kujenga mahusiano ya dini mbalimbali**. Wakristo wanapaswa kuendelea kujenga mahusiano ya heshima na ya kuaminiana na watu wa dini mbalimbali, ili kuwezesha kufahamiana kwa kina, kuridhiana na kushirikiana kwa ajili ya manufaa ya pamoja.

## MAPENDEKEZO

Mkutano wa tatu wa mashauriano ulioitishwa na WCC na PCID ya Kiti cha Kitume kwa kushirikiana na WEA na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka familia kubwa za imani ya kikristo (Wakatoliki, Waothodoksi, Waprotestanti, Wakiinjili na Wapentekoste), baada ya kufanyika tendo hili la ushirika wa kiekumeni katika kuandaa hati hii kwa ajili ya makanisa, vyombo ya kiimani vya kitaifa na kikanda na taasisi za kitume, hasa zile zinazofanya kazi katika muktadha wa mahusiano ya dini mbalimbali, unapendekeza kwa vyombo hivi:

1. **Kujifunza** juu ya masuala yaliyoainishwa katika hati hii na pale inapofaa kutengeneza miongozo ya utendaji juu ya ushuhuda wa kikristo unaoendana na muktadha mahsusi. Pale inapowezekana jambo hili lifanywe kwa ushirikiano wa kiekumene na kwa kushirikisha wawakilishi wa dini nyingine.

2. **Kujenga** mahusiano ya heshima na kuaminiana na watu wa dini zote, hasa kwa ngazi za kitaasisi kati ya makanisa na jumuiya zingine za kidini, kwa kujikita katika mazungumzano endelevu na dini mbalimbali kama seehemu ya wajibu wa kikristo. Katika muktadha mwingine, pale ambapo migogoro na migongano ya muda mrefu imejenga kudhaniana vibaya na kutoaminiana kati na baina ya jumuiya, mazungumzano kati ya dini inaweza kutoa fursa mpya ya kutatua

migogoro, kujenga tena misingi ya haki, kuponya kumbukumbu, upatanisho na kujenga amani.

3. **Kuhimiza** wakristo kuimarisha utambulisho wao wa kidini na wa kiimani na wakati huohuo kukuza ujuzi na uelewa wao juu ya dini tofauti, wakifanya hivyo huku wakizingatia mitazamo ya waamini wa dini hizo. Wakristo wanapaswa kujiepusha kutafsiri vibaya imani na matendo ya kiimani ya watu wa dini zingine.

4. **Kushirikiana** na jumuiya za dini zingine katika utetezi juu ya masuala ya haki na mustakabali wa pamoja na, pale inapowezekana, kusimama pamoja kwa mshikamano na watu walio katika hali na mazingira ya migogoro.

5. **Wito** kwa serikali zao kuhakikisha uhuru wa kuabudu unaheshimiwa kikamilifu, tukitambua kwamba katika nchi nyingi taasisi za dini na watu wanazuiwa kutekeleza utume wao.

6. **Kusali** kwa ajili ya jirani zao na kwa mustakabali wao, tukitambua kwamba sala ni sehemu ya msingi wa kile tulicho na wa kile tunachofanya na wa utume wa Kristo.

## KIAMBATISHO: Asili ya hati hii

1. Katika ulimwengu wa leo kuna ushirikiano unaokua baina ya wakristo na baina ya wakristo na wafuasi wa dini mbalimbali. Baraza la Kipapa la Mazungumzano na dini zingine (PCID) na Programu ya Baraza la Makanisa Duniani juu ya Mazungumzano na dini mbalimbali na Ushirikiano (Programme on Interreligious Dialogue and Co-operation - IRDC) (WCC-IRDC) wana historia ya ushirikiano huo. Mifano ya mada ambazo PCID/IRDC zimeshirikiana katika miaka ya nyuma ni: Ndoa baina ya watu Dini mbalimbali (1994-1997), Sala baina ya Dini mbalimbali (1997-1998) na Dhima ya Dini ya Kiafrika (2000-2004). Hati hii ni matokeo ya kufanya kazi pamoja.

2. Katika ulimwengu wa leo inazidi kukua migogoro baina ya dini mbalimbali, migogoro ilifikia viwango vya ghasia na upotevu wa maisha ya watu. Siasa, uchumi na masuala mengine yanachangia migogoro hii. Wakati mwingine wakristo wanahusika katika migogoro hii, kwa utashi wao au bila utashi wao, kama wale wanaoteswa au kama wale wanaoshiriki katika ghasia. Katika kujibu hali hii PCID na IRDC ziliamua kulizungumzia suala hili kwa lengo la kutoa

mapendekezo yanayokubalika kwa pande zote ili kuwasaidie wakristo katika ushuhuda wao. Baraza la Makanisa Duniani (WCC) na Mazungumzano baina ya dini na Ushirikiano (IRDC) ililialika Shirikisho la Ulimwengu la Makanisa ya Kiinjili (WEA) kushiriki katika mchakato huu na wao walishiriki kwa furaha.

3. Mwanzoni, ilifanyika mikutano miwili. Mkutano wa kwanza ulifanyika Lariano, Italia kuanzia tarehe 12 – 18 Mei 2006 uliokuwa na mada: “Kutathmini Hali Halisi” ambapo wawakilishi kutoka dini mbalimbali walichangia mawazo na uzoefu wao juu ya suala la wongofu. Sehemu ya tamko la mkutano huo linasomeka hivi: “Tunatamka kwa dhati kwamba, wakati kila mmoja ana haki ya kuwaalika wengine kuzijua imani zao, hili halipaswi kutekelezwa kwa kukiuka haki na hisia za kidini za wengine. Uhuru wa kuabudu unawapatia wote wajibu usiopingika wa kuheshimu imani za wengine, pasipo kamwe kudhalilisha, kukashifu au kuzitafsiri ovyo imani za wengine ili kuonesha ukuu wa imani yetu.”

4. Mkutano wa pili ulifanyika mjini Toulouse, Ufaransa, kuanzia tarehe 8 – 12 Agosti 2007, kutafakari masuala haya haya. Maswali juu ya Familia na Jumuiya, Heshima kwa wengine, Uchumi, Masoko na Ushindani, Ghasia na Siasa yalijadiliwa kwa kina. Masuala ya kichungaji na umisionari yanayoendana na hoja hizi yakawa msingi wa tafakari ya kiteolojia na misingi inayoelezwa katika hati hii. Kila suala ni muhimu kwa nafasi yake na lina haki ya kuangaliwa kwa makini katika mapendekezo haya.

5. Washiriki wa mkutano wa tatu walikutana Bangkok, Thailand, kuanzia 25 – 28 Januari 2011 na kukamilisha hati hii.